IBADA YA HIJA NA VILE INAVYOTEKELEZWA

Na Sheikh Nassor Khamis

MWANAMKE hafai kusafiri safari ya kukusuru sala peke yake ila awe na maharimu yake. Maneno hava yana maana kwamba mwanamke, wa Kiislamu haifai kwake yeye kusafiri kwenda hija bila ya kowa na maharimu yake (mtu anayemuhusu).

Na maharimu yake ni yule ambaye si halali kwake yeye kumwoa kabisa, nao ni, baba, mtoto, kaka, mtoto wa kaka na mtoto wa hao. Ama shemegi au mume wa shangazi au mume wa mama mdogo au mkubwa kao hawawi maharimu kwa maana shemegi anaweza kuja kumuoa shemegi yake baada ya mumewe ama kuachana.

Mtu alopaswa na Hija halafu asihiji mpaka akafa.

Mtu yeyote aliyepasiwa na hija, yaani iliyemuwajibikia kisha asihiji mpaka akafa itawapasa wale warithi watoe fungu katika zile mali zake zitakalomwezesha mtu mwengine kwenda kumhijia. Ni sawa hija hiyo awe ameiwacha kusudi ama si kusudi. Mwanamke mmoja wa kisahaba alikwenda kwa Mtume SAW na kumuuliza hivi, Mamangu aliweka nadhiri ya kuhiji, lakini alikufa kabla hajaitekeleza nadhiri yake. Jee nimuhijie? Akajibu Mtume ndiyo muhijie, waonaje lau kama mamako alikuwa na deni la watu, jee ungalilipa? Kwa hivyo mlipeni Mwenyezi Mungu, kwani Mwenyezi Mungu ndiye anayefaa kulipwa. (Bukhari).

Nguzo za Hija

Nguzo za hija ni zile ambazo kwazo huwa hija imesihi na atakapoiwacha moja tu basi hija hiyo hairakibishiki kwa kitu chengine, bali huwa imebatilika moja kwa moja ni lazima ailipe mwaka utakaofata.

Na nguzo za hija ni kama zinavyofata: Kuhirimia, nako ni kukusudia pamoja na kunuwia. Pili ni kusimama Arafa, kwa kumuomba Mwenyezi Mungu. Tatu ni kutembea kati ya Safa na Marwa. Na ya nne, ni kutufu Tawafa ya Ifadha, nayo ni ile inayofanywa baada ya kurudi Muzdalifa na kurusha vijiwe na kunyoa na kuchinja mtu aende Makka akafanye Tawafu. Zikikosekana nguzo hizi basi hija haikusihi, na ni lazima ilipwe mwakani. Ama mengine yaliyosalia huitwa ni wajibati za hija, moja likikosekana basi hija hurekibishwa kwa kumwaga damu yaani kuchinja mnyama.

Sehemu ambazo anayetaka kuhiji hawezi kuzipita bila ya kwisha nuia Hija au Umra:

Sehemu hizo ni I Dhul Hulefa, nayo ni sehemu ya wakaazi wa Madina na kila atakayepitia huko, napo ni nje ya mji wa Madina Kusini, yapata kama kilomita kumi na nane, na hapo ndipo alipohirimia Mtume SAW mwaka aliohiji. II, Dhati Irq, nayo ni sehemu ya watu wanaotoka Iraq, na mwenyekupitia huko, napo ni kaskazini mashariki ya Makka, ni kama kilomita tisini na nne. III, Juhfa, nayo ni sehemu ya watu wanaotoka Misri, Shamu na Ulaya. Na kijiji hiki kiliangamia na sasa watu wanahirimia kutoka Rabigh nacho ni kijiji kilichoko kaskazini magharibi ya Makka umbali wa kilomita 204. IV, Qarnu Manazil, nayo ni sehemu ya kuhirimia watu wanaotoka Najdi yaani watu wanaotoka Riyadh, Damam na kwengineko huko, nako ni mashariki ya Makka yapata kilomita 94, na pia ni sehemu ya kila atakayepitia huko. V, Yalamlam nayo ni sehemu ya watu wanaotoka Yemen na kila atakayepitia huko, nako ni kusini ya Makka yapata kilomita 94.

Hivi ndivyo alivyopanga Mtume wetu SAW na yeyote anayekusudia Hija au Umra si halali kwake kuzipita sehemu hizi bila ya kuhirimia, na akipita ni lazima arudi akaanze tena upya, bila ya hivyo hija yake ama Umra yake kabisa haitosihi.

Ama walioko ndani ya sehemu hizo au wale wanaoishi Makka, hapo wanapokaa ndipo watakapoanza nia ya Hija na Jeddah yahesabiwa ni Makka.

(Itaendelea).

Rais Moi akimpokea Rais wa Malawi Dr. Kamuzu Banda alipsimama Nairobi akiwa njiani kuelelkea wingereza. PICHA: K.N.A.

Waislamu wa Nakuru watuandikia

NA FARAJ DUMILA

WAISLAMU wa Rift Valley wamejitolea kikamilifu kushiriki katika maendeleo ya nchini na kujenga Taifa la Kenya kwa njia zote wanazoweza ili kuhakikisha kudumu kwa ufanisi chini ya maongozi ya Philosophia ya Nyayo.

Haya yameelezwa na Mwenyekiti wa Chama cha Waislamu wa Rift Valley, Sheikh Yahya Said baada ya kumkabidhi Mkuu wa Wilaya ya Nakuru, Bw. B. K. Ogol msaada wao kuwapelekea wale waliosibiwa moto huko Lamu. Mchango wenye thamani ya shilingi elfu kumi na mbili ulitolewa na chama hiko.

Mabibi wa Waislamu wa Nakuru nao walishiriki katika mchango huo kwa kutoa nguo zenye ya shilingi elfu|nane.

Waislamu hao walithibitisha imani yao, mapenzi yao na utiifu wao kwa Mtukufu Rais Moi, Serikali na Chama cha Kanu na kutoa ahadi kwamba wakati wowote wao wako imara kutoa utumushi wowote unaotakiwa na Serikali katika kuleta mafanikio yanayohitajiwa na wananchi wenye nia njema.

Waliokosa vya Arabuni wapita wakiropokwa

Na Abdulrahman Sheriff

NI sasa ya kila mwandishi wa makala ya gazeti lolote kuhakikisha yale atakayoyaandika yanakuwa ya kweli na yenye ushahidi wa kutosha ili anapohitajika kuthibitisha afanye hivyo. Ingawa sasa ni muda mrefu umepita, karibu kufika mwezi, imenilazimu nijibu makala ya mwandishi wa gazeti hili aliyezungumza kwa kirefu kuhusu tende, mazulia na mashafu yalivoletwa kwa ajili ya Waislamu.

Kwanza, nilishangazwa mno na maoni ya mwandishi wetu alipolaumu wanachuoni wa Mombasa kwa kutojitokeza kujaza nafasi ya kadhi wa mji. Kutokana na lawama na yale aliyoyazumgumza Bwana huyum yaonyesha na kueleka yeye amewashinda wanavyuoni wote.

KIISLAMU

Basi namuuliza mwandishi huyu kwa nini yeye asijitokeze na kujaza nafasi hiyo? Ikiwa yeye anaona wanavyuoni wengine wanakwenda kinyume cha matakwa ya dini yetu ya Kiislamu, kwa nini hajitangazi kama mtu aliyesafishika na mwenye kujua zaidi?

Mafunzo ya dini yetu ya Kiislamu yanatufunza kuheshimu wacha-mungu na watu waliotupita umri na vashangaza Mwandishi wetu kujitokeza kumkashifu na kumsingizia mwanachuoni ambaye hamwingilii mtu. Yataka afahamu kwamba ikiwa yeye aliona kuna kosa lilofanyika, kama Muislamu aliyejisafisha, haikuwa wajibu kwake kumwendea mkosaji na kumuonyesha njia badala ya kuandika na kumkashifu kwenye gazeti?

Kutokana na mwenendo wake huo, yaonyesha Bwana huyu hana uhakika wa yote yale aliyoyasema kuhusu vitu vilivyokuja bali alifanya hivyo kwa makusudi ya kumuharibia jina na sifa ya mcha-mungu ambaye habitaji maneno na mtu. Uhakika ulioko ni kwamba kama kuna msikiti ambao haukupata tende, basi lawama ni za wasimamizi wa msikiti huo kwani hupinga vyakula aina yoyote visiliwe misikiti.

Sikubaliani kabisa na matamshi ya mwandishi wetu aliyoyasema kwamba eti vifaa pamoja na fedha zimekuwa vikigawiwa kwa wale wenye damu ya Mtume pekee. Je, ana uthibiti gani kuhusiana na madai hayo? Na ikiwa anataka ukweli, angelitembelea madrassa zote na kuelewa ukweli juu ya jambo hilo badala ya kuchukua shauri la "marafiki" zake na kujiandikia lawama zisizo za msingi.

Kuhusu madai yake ya fedha eti waligawiwa waalimu wawili watatu, nataka kumfahamisha kwamba jambo hilo hakulifanyia uchunguzi kabisa kwani kama angelifanya hivyo, angelijionea mwenyewe mambo yaliyofanyiko. Yasikitisha kuona kwamba ikiwa alifahamishwa vibaya, sasa lawama zinamfikia yeye ambaye hakutumia busara katika kuhakikisha ukweli juu ya jambo hilo.

Na nina ushahidi wa kutosha wa kumfahamisha mwandishi huyu kuwa hakukuwa na ubaguzi wa aina yoyote uliofanyika kuhusiana na madai yake eti wengi walionufaika walikuwa wenye damu ya Mtume Mohammed (SAW). Waalimu wengu nilowadadisi walinifahamisha kuchukizwa kwa ripoti hiyo na wakamlaumu mwandishi kwa kutoa lawama zisizo na msingi.

MSAMAHA

Dini yetu inatufundisha upendo na umoja na Muislamu unawajibika kumuelekeza njia yule unayekifikiria amepotea badala ya kuamua kumkashifu.

Lazima mwandishi akubali kuomba msamaha ikiwa ameshindwa kuthibitisha kuhusu lawama alizotoa ama sivyo, athibitishe mahali popote atakapotakikana kufanya hivyo!

Ask to see the Dulux 1982 colour fashion range for a new world of natural colours.

Dulux*

Dulux*

SUPERCOVER EMULSION AND GLOSS

Dulux. It looks great. And goes on looking great. Because Dulux is durable. Resistant to the heat of the sun and the lashing rain, Dulux endures through the harshest weather.

Dulux is economical too because a Dulux surface lasts and lasts and lasts . . . And when the last smooth brush strokes are made, Dulux gives you the most handsome surface, inside or out.

Dulux emulsion and Dulux gloss are premium grade products based on a worldwide paint technology and carefully formulated especially for Kenyan conditions.

Professionals in the building industry specify Dulux because Dulux Paints are supreme in quality, durability and beauty.

After all, they have their reputations to uphold.

* DULUX IS A REGISTERED TRADE MARK OF © IMPERIAL CHEMICAL INDUSTRIES U.K. AND IS MANUFACTURED IN KENYA UNDER LICENCE BY

Twiga paints

People and paints you can rely on

AVAILABLE FROM HAPA LIMITED NAIROBI DAR-ES-SALAAM ROAD TELEPHONE 556019/557030 AND HAPA LIMITED KILINDINI ROAD MOMBASA TELEPHONE 313517

MAIN DISTRIBUTORS:
KIPSIGIS TRADERS KERICHO ● SHABAWA HARDWARE KISII
R F MEHIDA KAKAMEGA ● WARENG HARDWARE ELDORET
CHAI MOTORCYCLES AND HARDWARE KERICHO
COMPTRA LIMITED KITALE ● FARM AND HARDWARE KERICHO
CECYPO TIMBER AND HARDWARE KISUMU
RAINBOW GENERAL STORES KISUMU
KITALE STEELWARES KITALE ● AHAMED YAKUB & SONS MERU
KITUI COMMERCIAL DISTRIBUTORS KITUI